# TAWA BULLETIN

Toleo Na. 2 (Oktoba- Disemba 2025)



# YALIYOMO


TUZINGATIE UTU, SHERIA NA HAKI KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA ULINZI WA RASILIMALI ZA TAIFA- DKT KIJAJI | 01

DC WANGING'OMBE AFUNGA MAFUNZO YA KUKABILIANA NA GHASIAKWA ASKARI WA TAWA | 03

KAMPUNI YA MAGELLAN GENERAL TRADING LLC YAKABIDHI GARI KWA TAWA | 05

AWF YAIKABIDHI TAWA JENGO LA KIKOSI CHA MBWA NUSA | 06

KAMISHNA KABANGE AFUNGUA MAFUNZO YA WAENDESHA MASHTAKA WA TAWA | 08

KAIMU KAMISHNA WA UHIFADHI TAWA "AFUNGUA KIKAO KAZI CHA MENEJIMENTI YA TAWA | 09

SERIKALI IMEONESHA DHAMIRA YA DHATI KULINDA MAISHA YETU DHIDI YA MAMBA - WANANCHI MARA. | 10

TAWA YAKABIDHI MADAWATI 150 SHULE ZA MSINGI BARIADI. | 12

TAWA YAGUSA MAISHA YA WANANCHI MEATU | 14

TAWA YAKABIDHI BWENI LA WASICHANA SHULE YA SEKONDARI MCHENGERWA, RUFIJI | 16

DKT. KIJAJI AHIMIZA WANANCHI KUTUNZA MAENEO YA HIFADHI | 18

MISS WORLD CHINA ATEMBELEA HIFADHI YA MAKUYUNI WILDLIFE PARK | 12

ZAIDI YA WAGENI 140 KUTOKA MATAIFA MBALIMBALI WATEMBELEA HIFADHI YA KILWA KISIWANI | 20

HIFADHI YA MPANGA-KIPENGERE YAENDELEA KUWA LULU YA VIZAZI VIJAVYO | 23

TABORA ZOO YAENDELEA KUPOKEA MAKUNDI MBALIMBALI YA WATALII | 25

DKT. ABBAS AHAMASISHA WAKAZI WA DAR ES SALAAM KUSHIRIKI TAMASHA LA FUNGA MWAKA KIJANJA TALII | 26

MATUKIO KATIKA PICHA | 28



# Neno la ukaribisho

Ninayo furaha na heshima kubwa kukukaribisha msomaji wetu jarida la TAWA BULLETIN Toleo Na.2 Jarida hili linaakisi kwa vitendo juhudi, ubunifu na jitihada za. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ya uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, kuimarisha usalama, kukuza utalii na kugusa maisha ya jamii.

Katika kipindi hiki cha robo ya pili, Kwa heshima ya pekee, TAWA ilipokea ziara ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ashatu Kijaji (Mb), alipotembelea Makao Makuu ya TAWA mkoani Morogoro, ikiwa ni taasisi ya kwanza kuitembelea tangu ateuliwe na kuapishwa kuiongoza Wizara hiyo. Aidha, Mheshimiwa Waziri alitembelea Hifadhi ya Mpanga-Kipengere, hatua iliyozidi kuimarisha mwelekeo wa kisera na kiuongozi katika uhifadhi.

TAWA imeendelea kutekeleza kwa ufanisi shughuli mbalimbali zenye mwelekeo wa kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na kujenga uwezo wa rasilimali watu. Miongoni mwa shughuli hizo ni kufunga mafunzo ya kukabiliana na ghasia kwa Askari 60 wa Kikosi cha Mwitikio wa Haraka (RRT) mkoani Mbeya, pamoja na kufungua mafunzo ya waendesha mashtaka wa TAWA, hatua zinazolenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sheria na usalama wa maeneo ya hifadhi.

TAWA inaendelea kuthamini mchango wa wadau katika juhudi za uhifadhi. Katika robo hii, tumepokea msaada wa gari kutoka kwa Kampuni ya Magellan General Trading LLC kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika Hifadhi ya Mkungunero, pamoja na kukabidhiwa jengo la Kikosi cha Mbwa Nusa kutoka kwa wadau wetu AWF, lengo likiwa ni kuimarisha ulinzi wa rasilimali wanyamapori katika mipaka ya nchi, vituo vya forodha na viwanja vya ndege.

Kwa upande wa utalii na utangazaji wa vivutio vya Taifa, TAWA ilipata heshima ya kutembelewa na Miss World China katika Hifadhi ya Makuyuni Wildlife Park mkoani Arusha, pamoja na kupokea wageni 140 kutoka mataifa mbalimbali waliotembelea Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kale ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, Tamasha la Nyamapori Choma lililofanyika Tabora ZOO na Tamasha la Funga Mwaka Kijanja na TAWA jijini Dar es Salaam yalivutia mamia ya wananchi na wageni kutoka ndani na nje ya nchi, na kuchangia kwa kiasi kikubwa uhamasishaji wa uhifadhi na utalii wa ndani.

Katika kuimarisha uhusiano na jamii, TAWA iliendelea kugusa maisha ya wananchi kupitia utekelezaji wa miradi ya kijamii ikiwemo kukabidhi madawati 150 kwa shule za msingi wilayani Bariadi, kuzindua miradi ya ujenzi wa zahanati na ofisi mbili za walimu wilayani Meatu, pamoja na kukabidhi bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Mchengerwa wilayani Rufiji. Vilevile, elimu ya matumizi sahihi ya vizima moto ilitolewa kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa kama sehemu ya juhudi za usalama na uokoaji.

Robo hii pia ilishuhudia ushiriki wa TAWA katika matukio mbalimbali ya kitaifa ikiwemo mashindano ya SHIMMUTA na maonesho ya KOROSHO MARATHON mkoani Mtwara, sambamba na kuimarisha mshikamano wa ndani kupitia kikao cha Menejimenti ya TAWA kilichofunguliwa mkoani Mwanza.

Kwa ujumla, TAWA BULLETIN ya robo hii inaonesha dhamira ya dhati ya TAWA ya kuendelea kusimamia rasilimali za wanyamapori kwa weledi, kwa kushirikiana na wadau na jamii, huku tukihakikisha uhifadhi unakuwa chachu ya maendeleo ya Taifa na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

Nawashukuru watumishi wote wa TAWA, wadau wetu, Serikali na jamii kwa ushirikiano wao usioyumba. Tuendelee kufanya kazi kwa bidii, uzalendo na uwajibikaji kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mlage Yussuf Kabange
Kaimu Kamishna wa Uhifadhi
Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA

#TAWA TUNATEKELEZA

# TUZINGATIE UTU, SHERIA NA HAKI KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA ULINZI WA RASILIMALI ZA TAIFA- DKT KIJAJI

*Na. Joyce Ndunguru, Morogoro.*

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe.Dkt Ashatu Kijaji (Mb) aliwasisitiza watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuzingatia utu, sheria na haki katika utekelezaji wa majukumu ya ulinzi wa rasilimali za Taifa.
"Sisi watumishi wa umma tunapaswa kutoa huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa viwango huku tukizingatia haki, sheria na utu wa wananchi tunaowahudumia" alise,a Dkt. Kijaji.

Mhe. Dkt. Kijaji aliyasema hayo, Novemba 24,2025, katika ziara yake ya kwanza ya kikazi katika Ofisi za Makao Makuu ya TAWA zilizopo Mkoani Morogoro kwa lengo la kujifunza, kujionea jinsi shughuli za uhifadhi na utalii za TAWA zinavyofanyika na kujitambulisha kwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.




Pia, Dkt. Kijaji alisistiza kuendelea kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori katika maeneo ya hifadhi kwa kuongeza ufanisi katika doria, ujenzi wa vituo vya askari na matumizi ya teknolojia kama ndege nyuki (drones) na visukuma mawimbi (GPS Collars).

Sambamba na hayo, Mhe.Dkt. Kijaji alizindua vitendea kazi ambavyo ni magari (4) ya shughuli za doria, pikipiki (33) kwa ajili ya shughuli ya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na pikipiki ya miguu mitatu (Bajaji) iliyokabidhiwa kwa Askari wa Uhifadhi, Elihuruma Rashid aliyepata changamoto za kiafya akiwa katika kutekeleza majukumu yake ya kikazi.

Naye, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Hamad Chande (Mb) alisema kwamba, vitendea kazi hivi vilivyozinduliwa ni jitihada zilizofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza sekta ya wanyamapori.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAWA, Mej.Jen (Mstaafu) Hamis Semfuko alisema kuwa Bodi itahakikisha kuwa maelekezo yaliyotolewa yanatekelezwa kwa ubunifu na weledi wa hali ya juu.

Aidha, Mej. Jen (Mstaafu) Semfuko aliongeza kuwa TAWA itaendelea kuhakikisha kuwa jamii zinazopakana na hifadhi zinafaidika kutokana na rasilimali zilizopo katika maeneo hayo.

Awali, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mlage Yussuf Kabange alisema TAWA ina jukumu kubwa la kuhakikisha rasilimali za wanyamapori zinalindwa katika maeneo yanayoisimamia yakiwemo Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu hivyo kuongezeka kwa vitendea kazi hivi kutachagiza ufanisi wa shughuli za doria katika maeneo mbalimbali.
Kadhalika, Kamishna Kabange aliongeza kuwa jitihada mbalimbali zilizofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kukuza sekta ya utalii zimeweza kuongeza idadi ya watalii kutoka katika mataifa ambayo awali yalikuwa hayana idadi kubwa ya wageni.

"Jitihada hizi za Mhe. Rais zimewezesha TAWA kupata kampuni ya mwekezaji wa kwanza kutoka Nchini China aliyewekeza katika shughuli za uwindaji wa kitalii," alisema Kamishna Kabange.

Katika ziara hii, Mhe. Kijaji aliambatana na Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mhe. Hamad Chande, Katibu Mkuu wa Wizara ya Malisili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi na Viongozi wengine wa Wizara ya Malisili na Utalii.



# DC WANGING'OMBE AFUNGA MAFUNZO YA KUKABILIANA NA GHASIA KWA ASKARI WA TAWA

*Na. Beatus Maganja, Njombe.*



Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Mhe. Zacharia Mwansasu, Oktoba 8, 2025 alifunga rasmi mafunzo siku 10 ya kukabiliana na ghasia (Anti-Riot) kwa kikosi maalum cha Askari 60 wa mwitikio wa haraka wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA (RRT) katika Kituo cha Mafunzo cha Welela Mkoani Njombe, akisisitiza umuhimu wa nidhamu, weledi na uzingatiaji wa sheria katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo, Mhe. Mwansasu alisema "Serikali inatambua changamoto zinazowakabili Askari wa Uhifadhi, ikiwemo hatari wanazokutana nazo katika kulinda rasilimali za taifa, ambapo baadhi wamejeruhiwa na wengine kupoteza maisha." Na kuongeza kuwa mafunzo hayo yaliyotolewa na TAWA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi yatasaidia kuongeza ufanisi na uwezo wa askari kukabiliana na ghasia kwa kutumia nguvu ya kadiri bila kuathiri haki za binadamu.

Mhe. Mwansasu alieleza kuridhishwa na umahiri uliooneshwa na Askari hao katika mafunzo ya vitendo, yakiwemo matumizi ya mabomu ya machozi, upekuzi, ukamataji watuhumiwa na mazoezi ya ukakamavu. Alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kutoa mafunzo hayo na kuomba kuendeleza ushirikiano huo ili kuboresha utendaji wa Jeshi la Uhifadhi.
Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alitumia fursa hiyo kulaani vikali vitendo vya baadhi ya wananchi kuvamia na kuwashambulia Askari wa Uhifadhi wakiwa kazini. Aliwataka wananchi kuacha mara moja kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa na kuheshimu sheria za uhifadhi.

Akihitimisha hotuba yake, Mhe. Mwansasu aliipongeza Menejimenti ya TAWA kwa kuandaa mafunzo hayo na kuwataka wahitimu kutumia ujuzi walioupata kuboresha uhifadhi na kuongeza mapato kupitia utalii.

Kwa upande wake, Naibu Kamishna wa Uhifadhi – Huduma za Shirika, Thabit Maarufu, ambaye alimwakilisha Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiwezesha TAWA kifedha na kwa rasilimali watu, jambo linalozidi kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi nchini.

Aidha, Naibu Kamishna Maarufu alitoa shukrani kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, kwa kuruhusu wataalamu wa jeshi hilo kushiriki katika kutoa mafunzo ya kukabiliana na ghasia kwa Askari wa Uhifadhi. Alisema ushirikiano huo ni kielelezo cha mshikamano wa taasisi za ulinzi na usalama katika kulinda rasilimali za taifa.

Akizungumzia mipango ya mbele, alibainisha kuwa TAWA imeandaa mpango maalumu wa kuboresha mfumo wa mafunzo kwa kuongeza kozi mbalimbali ikiwemo mafunzo ya uokoaji majini na kuogelea kwa askari wake, ili kuwaongezea uwezo wa kukabiliana na changamoto katika maeneo mbalimbali ya uhifadhi.

Vilevile, alisema mamlaka imepanga kuongeza vifaa, kuboresha miundombinu ya mafunzo, na kuhakikisha Kituo cha Mafunzo cha Welela kinajengewa uwezo wa kuwa kituo bora na cha mfano nchini katika kutoa mafunzo ya kiusalama na uhifadhi.

Naye Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi wa TAWA, Abraham Jullu, alilishukuru Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori Duniani (WCS) Kwa mchango wake mkubwa linalotoa Katika shughuli za uhifadhi nchini hususani uwezeshaji wa mafunzo mbalimbali ikiwemo mafunzo ya RRT.

Kadhalika, Mratibu wa ulinzi wa program ya Ruaha Katavi WCS Bw. Stanley Mbilinyi alisema Shirika hilo linajivunia kushirikiana kwa ukaribu na TAWA katika kuanzisha na kuunga mkono vikosi vya kwanza vya RRT nchini Tanzania tangu mwaka 2015, pamoja na kushirikiana na taasisi hiyo kuandaa nyaraka muhimu za mipango na kujenga uwezo wa kutekeleza mbinu hii kitaifa.



# KAMPUNI YA MAGELLAN GENERAL TRADING LLC YAKABIDHI GARI KWA TAWA

*Na Joyce Ndunguru, Dodoma.*

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imekabidhiwa gari aina ya Toyota Land Cruiser Pick -up na Kampuni ya Magellan General Trading LLC, kwa ajili ya kuimarisha doria za ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori katika Hifadhi ya Mkungunero.
Akizungumza wakati wa makabidhiano ya gari hilo yaliyofanyika Oktoba 9,2025, katika Hifadhi ya Mkungunero, Mwakilishi wa Kampuni ya Megallan General Trading LLC, Ahmed Wasama alisema, wao kama wawekezaji mahiri katika Hifadhi ya Mkungunero wametoa gari hilo ili kuendelea kuimarisha shughuli za uhifadhi katika hifadhi hiyo.

Aidha, aliongeza kuwa Megallan itaendelea kushirikiana na TAWA katika masuala yote ya ulinzi, uboreshaji wa miundombinu ya utalii iliyopo katika Hifadhi sambamba na kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa vijiji vinavyoizunguka Hifadhi ya Mkungunero.
Kwa upande wake, Kamanda wa Hifadhi ya Mkungunero Floravick Kallambo ambaye alimwakilisha Kaimu Kamishna wa Uhifadhi - TAWA, aliishukuru uongozi wa Kampuni ya Megallan General Trading LLC, kwa kuwapatia gari hilo. Aidha, aliongeza kuwa gari hili litaboresha ufanisi katika shughuli za doria sambamba na kusaidia katika muitikio wa haraka wa matukio mbalimbali ya migongano baina ya wanyamapori na wananchi wanaopakana na hifadhi.

Hifadhi ya Mkungunero inapatikana katika Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma na imesheheni vivutio mbalimbali ikiwemo mandhari ya kuvutia na wanyamapori mbalimbali kama vile Tembo, Nyati, Twiga, Pofu, Kudu, Choroa na Pundamilia.






# AWF YAIKABIDHI TAWA JENGO LA KIKOSI CHA MBWA NUSA

*Na. Joyce Ndunguru, Arusha.*





Shirika la Kimataifa la African Wildlife Foundation (AWF) liliikabidhi rasmi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) majengo maalum kwa ajili ya Kikosi cha Mbwa Nusa (TAWA K9-UNIT) kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori katika maeneo ya Mipakani mwa Nchi, Vituo vya Ushuru wa Forodha na Viwanja vya Ndege vya Kilimanjaro na Arusha.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi na makabidhiano ya jengo la Kikosi cha Mbwa Nusa iliyofanyika Oktoba 21, 2025, katika Ofisi za TAWA, Kanda ya Kaskazini zilizopo jijini Arusha, Mgeni Rasmi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAWA, Mej.Jen (Mstaafu) Hamis Semfuko alisema Kikosi cha mbwa nusa (Sniffing dogs) ni nyenzo muhimu ambayo imekuwa ni msaada katika kudhibiti uhalifu unaohusiana na usafirishaji haramu wa nyara za Serikali na biashara haramu ya wanyamapori.

"Kikosi hiki kimekuwa msaada mkubwa hasa katika kudhibiti utoroshaji nyara kupitia mipakani, vituo vya usafirishaji na forodha," alisema Semfuko.

Mej.Jen (Mstaafu) Semfuko aliongeza kuwa TAWA itaendelea kukiimarisha Kikosi hiki kwa kuongeza idadi ya watumishi katika kikosi, kuongeza vitendea kazi pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa kikosi cha Mbwa Nusa.




Sambamba na hilo, Mej.Jen (Mstaafu) Semfuko aliwashukuru AWF kwa mchango wao uliowezesha ujenzi wa jengo la (TAWA-K9 UNIT). Aidha, ametoa rai kwa wadau wengine wa Uhifadhi kuendelea kushirikana na TAWA katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori.


Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la AWF, Pastory Magingi, alisema Jengo hili limekabidhiwa kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa sheria kupitia mbwa waliopatiwa mafunzo, sambamba na kuwapatia mbwa hawa makazi ya kudumu.

Pamoja na hilo, Bw. Magingi aliongeza kuwa AWF kwa kushirikiana na TAWA imeweza kuandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa vikosi vya mbwa wa uhifadhi.

Awali, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mlage Yussuf Kabange alisema mashirikiano mazuri yaliyopo baina ya TAWA na AWF yameweza kufanikisha ujenzi wa jengo hilo ambalo linajumuisha vyumba sita (6) vya mbwa, Ofisi, Stoo ya chakula, maliwato na eneo la wazi lenye uzio kwa ajili ya mazoezi ya mbwa.

Vilevile, Kamishna Kabange aliongeza kuwa pamoja na Mbwa Nusa (Sniffing dogs), TAWA imepanga kuanzisha Kikosi cha Mbwa wa ufuatiliaji (Tracking dogs) na kuanzisha Kituo cha mafunzo ya Mbwa (Dog Training Centre).
Naye, aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi TAWA, Segoline Tarimo ambaye alimwakilisha Kamanda wa Kanda ya Kaskazini alisema tangu kuanzishwa kwa Kikosi cha Mbwa, Kikosi kimepata mafanikio mengi ikiwemo kudhibiti uhalifu wa utoroshaji wa nyara kupitia kiwanja cha KIA na maeneo ya mipakani.
Kadhalika, aliongeza kuwa majengo haya yaliyokabidhiwa yatawezesha kikosi kufanya kazi katika mazingira bora na kwa ufanisi zaidi.

Hafla hiyo ya makabidhiano ya Jengo la Kikosi cha Mbwa Nusa, iliambatana na kusaini makubaliano (Memorandum of Understanding) baina ya AWF na TAWA. Makubaliano hayo yalijikita katika matumizi ya Mbwa Nusa na matumizi ya teknolojia katika kudhibiti uhalifu wa nyara za wanyamapori.



# KAMISHNA KABANGE AFUNGUA MAFUNZO YA WAENDESHA MASHTAKA WA TAWA

*Na. Joyce Ndunguru, Manyoni.*

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA, Mlage Yussuf Kabange alifungua mafunzo ya Waendesha Mashtaka wa TAWA wanaojihusisha na uendeshaji wa kesi za uhalifu wa wanyamapori mnamo Novemba 2025 katika Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida. Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Kamishna Kabange alisema mafunzo haya yamejikita katika kuimarisha shughuli za uendeshaji wa kesi mbalimbali zinazohusu uhalifu wa wanyamapori.

"Mafunzo haya ni muhimu, kwani yanaongeza ujuzi na ufanisi katika kukabiliana na uhalifu wa rasilimali yetu ya wanyamapori", alisisitiza Kamishna Kabange.
Sambamba na hilo, Kamishna Kabange aliongeza kuwa mafunzo haya yanaunganisha Waendesha Mashtaka wa TAWA pamoja na wataalamu wengine kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Jeshi la Polisi ili kukumbushana taratibu, kujadiliana changamoto za kiutendaji na kupitia mabadiliko muhimu ya sheria.
Kadhalika, Kamishna Kabange aliwataka washiriki kutumia kikamilifu fursa hii kwa kujifunza mbinu na mikakati itakayoboresha utendaji na kuongeza ushindi katika uendeshaji wa kesi. Pia aliwasisitiza kufanya kazi kwa uzalendo, uadilifu na kuzingatia sheria.

Vilevile, Kamishna Kabange aliishukuru Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ushirikiano wake mkubwa katika kuhakikisha kesi za uhifadhi zinamalizika kwa wakati na kwa mafanikio.

Mafunzo haya yamewakutanisha wataalamu mbalimbali kutoka TAWA, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Jeshi la Polisi

# KAIMU KAMISHNA WA UHIFADHI TAWA AFUNGUA KIKAO KAZI CHA MENEJIMENTI YA TAWA

*Na. Joyce Ndunguru, Mwanza.*

Kaimu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA, Mlage Yussuf Kabange alifungua kikao kazi cha Menejimenti ya TAWA kilichofanyika Disemba 13,2025 jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho kilichojumuisha Makamishna Wasaidizi Waandamizi, Makamanda wa Kanda na Wakuu wa Vituo vyote vya TAWA, Kamishna Kabange alisema lengo kubwa la kikao hiki ni kuboresha utendaji kazi ili kufikia malengo ya Mamlaka.

Kamishna Kabange alibainisha kuwa kikao kazi hiko kitajikita katika vipaumbele mbalimbali vitakavyoboresha maeneo ya utendaji kazi wa TAWA yakiwemo maeneo ya ulinzi na usimamizi wa wanyamapori, ukusanyaji wa mapato, migongano baina ya binadamu na wanyamapori, ujenzi wa miundombinu katika hifadhi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi hususan kwenye maeneo ambako askari wanafanya kazi.

Sambamba na hilo, Kamishna Kabange aliwasisitiza Makamishna Wasaidizi Waandamizi na Makamanda wa Kanda kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu unazingatia utu, sheria na haki bila upendeleo wowote.

Awali, akimkaribisha Kamishna wa Uhifadhi, Naibu Kamishna wa Uhifadhi anayeshughulikia Kurugenzi ya Huduma za Shirika, Maarufu Thabit Mkwaya alisema katika kikao kazi hiki viongozi wa Menejimenti watapata fursa ya kupitishwa katika mawasilisho mbalimbali yanayolenga kujenga uwezo wa kiutendaji, kuongeza ubunifu, kujitathmini, kubadili mitazamo na fikira za viongozi katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

Kamishna Maarufu aliongeza kuwa miongoni mwa mawasilisho hayo ni tathmini ya mpango mkakati wa Mamlaka (2021/22-2025/26) na maandalizi ya mpango mkakati mpya (2026/27-2030/31), Uongozi wa Kimkakati na Akili Hisia, Itifaki na Adili kwa viongozi, Afya ya Akili pamoja na Elimu ya Fedha na Uwekezaji.







# #TAWA NA JAMII



## SERIKALI IMEONESHA DHAMIRA YA DHATI KULINDA MAISHA YETU DHIDI YA MAMBA - WANANCHI MARA.

*Na Beatus Maganja, Mara*

Wananchi wa wilaya ya Bunda mkoani Mara wamekiri kuiona dhamira ya dhati ya Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA ya kutatua migongano baina ya wanyamapori na binadamu Kwa kuongeza Idadi ya vizimba, hatua inayotajwa kupunguza athari Kwa wananchi hao.
Kauli hiyo ilitolewa Oktoba 22, 2025 wakati wa ziara ya kukagua vizimba hivyo ikienda sambamba na utoaji elimu ya kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na wanyampori aina ya mamba na viboko iliyofanywa na maofisa wa TAWA mkoani humo.

Miongoni mwa wananchi aliyewahi kujeruhiwa na mamba, Kurwa Ryoba mkazi wa Kijiji cha Buzimbwe aliishukuru Serikali Kwa hatua hiyo ya kuongeza Idadi ya vizimba na alisema vizimba hivyo ni suluhisho muhimu katika kuokoa maisha ya wananchi, huku akiwasisitiza wananchi wenzake kutopuuzia kutumia vizimba hivyo ili wasije wakapata madhara aliyoyapata yeye
"Naishukuru sana Serikali kutujengea kizimba hiki, maana kabla hakijajengwa watu walipata madhara akiwemo ndugu yangu" alisema Ryoba.

"Wananchi wenzangu, kizimba hiki kimejengwa hapa lakini naona wengine wanadharau kukitumia, wakipata madhara wanaanza kuilaumu Serikali. Mimi nawashauri wajifunze kutoka kwangu, wachukue tahadhali watumie vizimba, Serikali imefanya maneno mazuri kutujengea vizimba" aliongeza mkazi huyo wa Kijiji cha Buzimbwe.



Afisa Habari wa TAWA Beatus Maganja alisema Kufuatia changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu nchini hususani katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Serikali kupitia TAWA katika bajeti ya Mwaka 2024/25 ilitenga zaidi ya shillingi million 210 Kwa ajili ya kuongeza Idadi ya vizimba vipya Saba (7) ambapo Kwa wilaya ya Bunda pekee vizimba vinne tayari vimekamilika na vinaendelea kutumiwa na wananchi.

Aidha alitoa rai Kwa wananchi hao kuwa na matumizi sahihi ya vizimba hivyo, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanavilinda ili viendelee kuwa msaada kwao.
"Hatujisikii furaha kusikia wananchi wanapata madhara ya wanyamapori hawa, hivyo ni muhimu mzingatie matumizi sahihi ya vizimba hivi Kwa ajili ya usalama zaidi ili kujiepusha athari hizo. Vilevile Serikali imetumia gharama kubwa kuvijenga, hivyo kila mmoja ana wajibu wa kuvilinda ili viendelee kuwa msaada " alisema Maganja.

Naye Afisa Uhifadhi Kutoka Kanda ya Ziwa, Sato Masinde aliwashauri viongozi wa vijiji kuunda Sheria ndogo ndogo ikiwa ni hatua muhimu ya kuhakikisha miundombinu hiyo inalindwa ipasavyo na kuendelea kuwanufaisha wananchi hao.



# TAWA YAKABIDHI MADAWATI 150 SHULE ZA MSINGI BARIADI.

*Na Beatus Maganja, Bariadi.*

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA Kwa kushirikiana na Kampuni ya uwindaji wa kitalii ya Bushman Safari Trackers imekabidhi madawati 150 Kwa shule za msingi tano (5) zinazopakana na Hifadhi ya Maswa wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu.

Shule zilizonufaika na mgao huo wa madawati ni pamoja na Shule ya Msingi Mwauchumu ambayo imepata madawati 30, damidami 30, Halawa 30, Mwabalizi 30 na Shule ya Msingi Nyawani ambayo nayo imepata madawati 30.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi madawati hayo iliyofanyika Novemba 21, 2025 katika Kijiji cha Halawa Kaimu Kamanda wa Uhifadhi kutoka TAWA Kanda ya Ziwa Mark Chuwa alisema madawati hayo yametokana na mradi wa Uwekezaji Mahiri (SWICA) ambao TAWA iliingia mkataba na Kampuni ya Kitalii ya Bushman Safari Trackers Ltd, ambapo mojawapo ya vipengere vya mkataba huo ni pamoja na kuhakikisha jamii zinazozunguka maeneo ya Hifadhi yaliyo chini ya usimamizi wa TAWA zinanufaika na rasilimali wanyamapori zinazopatikana katika maeneo husika.

"Hii ni sehemu ya utekelezaji wa mkataba huo, na ni manufaa ya moja Kwa moja ambayo inaenda Kwa jamii inayozunguka eneo letu" alisema Mark Chuwa.

Aidha Kamanda Chuwa ametoa rai Kwa wananchi wote wa Kanda hiyo kuendelea kushirikiana na Serikali kupitia taasisi hiyo katika kulinda rasilimali wanyamapori sambamba na kuwafichua wahalifu wote wanaofanya shughuli haramu za ujangili ndani ya hifadhi.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya jamii katika kitalu cha Maswa Kaskazini, Afisa Uhifadhi - Kitengo cha Ujirani Mwema Lusato Masinde alisema katika kuhakikisha jamii inayozunguka hifadhi ya Maswa inanufaika na shughuli za uhifadhi TAWA iliunda Kamati ya uwezeshaji jamii inayohusisha wahifadhi kutoka TAWA, Mwekezaji, Halmashauri ya Wilaya na mwakilishi wa wananchi ikiwa na majukumu ya kupanga, kutekeleza na kufanya ufuatliaji wa miradi itokanayo na mapendekezo ya wananchi.



Masinde alisema Kamati hiyo ilibaini kuwa kulikuwa na changamoto na uhitaji mkubwa wa madawati katika vijiji vyote sita na hivyo TAWA Kwa kushirikiana na Bushman Safari Trackers Ltd iliamua kutengeneza madawati 150 Kwa ajili ya Shule zilizopo katika vijiji husika.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Bariadi Mhe. Simon Simalenga alipokea na kukabidhi madawati hayo Kwa Shule zilizonufaika, aliishukuru na kuipongeza TAWA Kwa kushirikiana na Kampuni ya Kitalii ya Bushman Safari Trackers Kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kutatua changamoto za wananchi hususani kuboresha sekta ya elimu kwa shule za Mkoa wa Simiyu.

Aidha aliwataka wananchi hao kuona umuhimu wa kuendelea kulinda rasilimali wanyamapori zilizopo katika maeneo yao kwani zimekuwa na manufaa makubwa ikiwemo kuleta maendeleo na kutatua changamoto zinazowakabili.

"Ndugu wananchi, wanadau hawa wameleta madawati haya ni kwasababu Mwenyezi Mungu alitujalia kupata wanyamapori, kama tusingekuwa na wanyamapori basi leo hii hili tukio la kukabidhiwa madawati 150 lisingekuwepo"

"Niwapongeze sana TAWA na Mwekezaji Kampuni ya Bushman Kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kuboresha elimu nchini, niwaombe wananchi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda hifadhi zetu" alisema Mhe. Simalenga.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Halawa Boje Kalani aliwashukuru TAWA Kwa kuwapunguzia wananchi mzigo wa kuchangia kwa ajili ya kutatua changamoto ya ukosefu wa madawati kwenye shule yao ambapo alisema kila mwananchi angepaswa kuchangia shillingi 12,000/= jambo ambalo huwashinda wengi.

Vilevile Meneja wa Mradi wa Uwekezaji Mahiri (SWICA) Rubani Willness Minja ameipongeza Serikali kwa kuwashirikisha wawekezaji wazawa katika mkataba wa SWICA unaolenga kuimarisha uhifadhi, kuwanufaisha wananchi na kuongeza mapato zaidi kwa Serikali





# TAWA YAGUSA MAISHA YA WANANCHI MEATU

*Na Beatus Maganja, Meatu*

Wananchi wa Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu wanatarajiwa kuondokana na adha ya upatikanaji wa huduma za afya na elimu baada ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kwa kushirikiana na Kampuni ya Kitalii ya Mwiba Holdings Ltd. kuibua miradi ya ujenzi wa zahanati moja katika Kijiji cha Matale, madarasa manne na ofisi mbili za walimu katika Kijiji cha Mbughayabanyha.

Hatua hii ni sehemu ya jitihada za Serikali kupitia TAWA na wadau wake katika kutatua changamoto za wananchi na kuhakikisha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi zinanufaika moja kwa moja na rasilimali za wanyamapori.

Akizungumza katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi katika miradi hiyo Novemba 25, 2025 iliyofanyika katika vijiji hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Meatu Mhe. Fauzia Ngatumbura aliipongeza TAWA Kwa kushirikiana na Kampuni ya Mwiba Holdings Ltd. kwa Kuibua miradi yenye tija na manufaa makubwa inayozingatia utu wa mtanzania na kutoa rai kwa wananchi kuthamini, kulinda na kutunza miradi hiyo.





"Niwapongeze sana TAWA Kwa kushirikiana na wadau wenu kwa usimamizi mzuri wa miradi hii na Kazi kubwa mliyoifanya, ambapo Kwa kushirikiana na wananchi mmeweza kuibua miradi kila Kijiji Kwa kuzingatia mahitaji ya maeneo husika" alisema Mhe. Fauzia. "Wito wangu kwenu wananchi ni kwamba muendelee kuuenzi uhifadhi, kutoa ushirikiano Kwa wahifadhi katika kulinda hifadhi zetu, kwasababu kupitia hifadhi hizi tunaweza kupata fedha za kigeni na fedha Kwa ajili ya miradi mingine mingi" aliongeza Mkuu huyo wa Wilaya ya Meatu.

Ujenzi wa zahanati hiyo ambayo imefikia asilimia 63 unatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya akina mama na watoto kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, huku madarasa na ofisi za walimu zilizofikia asilimia 75 zikitarajiwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo inayotokana na shughuli za uhifadhi na utalii kupitia Uwekezaji Mahiri (SWICA) ndani ya hifadhi ya Maswa iliyoanza Oktoba 25, 2025 na kutarajiwa kukamilika Disemba 2025, Afisa Uhifadhi kutoka TAWA Kanda ya Ziwa Lusato Masinde alisema ujenzi wa zahanati ambayo itakuwa na wodi ya mama na mtoto, OPD na RCH itagharimu kiasi cha zaidi ya shillingi millioni 286 huku ujenzi wa madarasa manne na ofisi mbili za walimu ukigharimu kiasi cha shillingi millioni 216.7.

Baadhi ya wananchi wameeleza furaha yao kutokana na miradi hiyo, wakisema kuwa imefika wakati muafaka na itaongeza imani na matumaini kwa Serikali yao huku TAWA ikiahidi kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Kupitia miradi hii, Meatu inatarajiwa kupiga hatua kubwa katika kuboresha huduma za kijamii na kuimarisha uhusiano kati ya wananchi na TAWA.

# TAWA YAKABIDHI BWENI LA WASICHANA SHULE YA SEKONDARI MCHENGERWA, RUFIJI

*Na Beatus Maganja, Rufiji, Pwani.*

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ilikabidhi bweni jipya la wasichana katika Shule ya Sekondari Mchengerwa iliyopo Kata ya Ngarambe wilayani Rufiji mkoani Pwani ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya elimu, hasa kwa mtoto wa kike.

Bweni hilo ambalo ujenzi wake umegharimu zaidi ya shilingi milioni 252, limejengwa kwa ushirikiano kati ya TAWA na Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori (Frankfurt Zoological Society – FZS) chini ya ufadhili wa Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya watu wa Ujerumani (KfW), lilikabidhiwa likiwa na jumla ya vitanda 40 aina ya "double decker", magodoro 80, huduma ya maji safi, pamoja na umeme unaohudumia wanafunzi wapatao 80.

Mbali na bweni hilo, TAWA pia ilikabidhi darasa moja la kisasa likiwa na meza 45 na viti 45 vya wanafunzi pamoja na viti vinne na meza mbili za walimu katika shule ya Sekondari Mwaseni wilayani humo, vyote vikiwa na thamani ya shillingi millioni 60 na kufanya miradi yote miwili iliyokabidhiwa kuwa na thamani ya zaidi ya shillingi millioni 312

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano na uzinduzi wa miradi iliyofanyika wilayani humo Disemba 03, 2025, Mwakilishi wa Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Abraham Jullu alisema ujenzi wa mradi huo uliotokana na mradi wa dharura wa kupambana na majanga ya UVIKO - 19 (ERB) unalenga kuondoa changamoto ya mazingira duni ya kujisomea na kujifunzia kwa wanafunzi hususani wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwenda shuleni na hivyo kuwa hatarini dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

"TAWA inaendelea kushirikiana na Serikali na wadau wa maendeleo kuhakikisha jamii zinazozunguka maeneo yetu ya hifadhi zinapata huduma bora za kijamii. Uwekezaji huu katika elimu ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wetu wa kijamii kupitia shughuli za uhifadhi, kujenga mahusiano mazuri na jamii ili kuhakikisha, usalama, utulivu na ustawi wao katika nyanja mbalimbali" alisema.



"Bweni hili litaboresha kwa namna kubwa mazingira ya masomo Kwa wanafunzi wa kike, litawaweka mahali salama, Karibu na shule na litawapa muda zaidi wa kujisomea na kupumzika bila hofu ya wanyama hatari wala safari ndefu. Hii ni hatua muhimu katika kuongeza ufaulu, usawa na fursa za elimu na kulinda haki ya mtoto wa kike kupata mazingira bora ya kujifunzia" aliongeza

Naye Mkurugenzi Mkaazi wa FZS Dkt. Maurus Msuha alisema shirika hilo litaendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania katika suala la uhifadhi na kushirikiana katika kuboresha huduma za elimu kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha alibainisha kuwa uwekezaji katika elimu ya mtoto wa kike ni msingi wa maendeleo ya jamii.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji Mhe. Luteni Kanali Fredrick Komba aliishukuru TAWA na wadau wake kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kutatua changamoto mbalimbali za kijamii hususani katika kuboresha sekta ya elimu wilayani humo sambasamba na kudumisha mahusiano mazuri na jamii zinazozunguka Hifadhi ya Selous.

Vilevile aliipongeza Serikali ya Ujerumani Kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kufanikisha masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kimaendeleo.
“Hatua hii itasaidia kuongeza ufaulu, kuboresha nidhamu na kupunguza utoro miongoni mwa wanafunzi wa kike. Tunaishukuru TAWA, FZS na Serikali ya Ujerumani kwa kuona umuhimu wa kuwekeza katika elimu ya watoto wetu,” alisema Luteni Kanali Fredrick Komba

Wazazi, walimu, wanafunzi na viongozi wa vijiji vya Ngarambe na Mwaseni walipongeza juhudi hizo wakisema ujenzi wa miradi hiyo ni uthibitisho wa dhahiri kuwa TAWA haitumii tu rasilimali za taifa Kwa ajili ya uhifadhi, bali inarejesha sehemu ya faida hizo Kwa jamii zinazowazunguka

Aidha walisema miradi hiyo imekuwa faraja kubwa kwa wanafunzi wa kike ambao hapo awali walikabiliwa na changamoto ya kutembea masafa marefu, usalama na mazingira duni ya kujisomea pia ujenzi wa darasa utapunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi darasani.







# DKT. KIJAJI AHIMIZA WANANCHI KUTUNZA MAENEO YA HIFADHI

*Na. Joyce Ndunguru, Njombe.*

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) amewahimiza wananchi wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi ya Mpanga Kipengere kutunza hifadhi hiyo kwa kuzingatia kuwa, takribani vijiji 96 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na vijiji/miji vya Ilembula, Igawa na Igwachanya vinanufaika na miradi ya maji ambayo chanzo chake ni ndani ya hifadhi ya Mpanga Kipengere.

Mhe. Dkt. Kijaji aliyasema hayo Disemba 17,2025, alipotembelea Hifadhi ya Mpanga Kipengere iliyopo katika Mikoa ya Njombe na Mbeya kwa lengo la kujionea jinsi shughuli za uhifadhi zinavyofanyika, ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya kikazi katika maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

“Tusipohifadhi na kuitunza hifadhi yetu hii ya Mpanga kipengere tutakosa maji lakini tutakosa manufaa mengine ya kijamii na kiuchumi tunayopata kupitia hifadhi hii, hivyo niwaombe vijiji vyote vilivyotuzunguka tuweze kuhifadhi kwa pamoja”, alisema Waziri Kijaji.

Sambamba na hilo, Waziri Kijaji aliisisitiza TAWA kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa za uwekezaji na mazao mbalimbali ya utalii katika Hifadhi hiyo.

“Tuje na vivutio vipya vya utalii vilivyomo ndani ya hifadhi yetu , lakini pia tuwaite wawekezaji, tuwauzie fursa ili wawekeze nasi,” aliongeza Waziri Kijaji

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Hamad Chande (Mb) aliwataka watanzania wanaoishi Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo ukanda huu yakiwemo Maporomoko maarufu ya maji ya Kimani yanayopatikana ndani ya Hifadhi ya Mpanga Kipengere.

Naye, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, Mlage Yussuf Kabange alisema TAWA imeboresha miundombinu mbalimbali ya utalii na utawala iliyopo ndani ya hifadhi ikiwemo ujenzi wa banda za watalii, kambi ya watalii, ofisi, ujenzi madaraja pamoja na barabara.

Kuhusu mahusiano na jamii, Kamishna Kabange alisema vijiji vinavyoizunguka vinanufaika na miradi ya maji ambayo chanzo chake ni ndani ya hifadhi ya Mpanga Kipengere. Aidha, mito iliyopo ndani ya Hifadhi ya Mpanga Kipengere ni vyanzo muhimu vya maji ya skimu za umwagiliaji za Igomelo, Malangali, Wangama, Wangamiko na Imalilo ambazo zinanufaisha jamii moja kwa moja.Katika ziara hiyo ya kikazi, Waziri Kijaji aliambatana na Naibu Waziri Wa Maliasili na Utalii, Mhe. Hamad Chande, Naibu Katibu Mkuu (Utalii), Nkoba Mabula na viongozi wengine wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Hifadhi ya Mpanga Kipengere inayopatikana Mikoa ya Njombe na Mbeya ni hifadhi iliyosheheni vivutio vingi likiwemo Maporomoko ya Maji takribani 50 na uwanda uliosheheni maua ya kuvutia.



# #TAWA MAISHA BILA STRESS

# MISS WORLD CHINA ATEMBELEA HIFADHI YA MAKUYUNI WILDLIFE PARK

*Na Beatus Maganja, Arusha*

Hifadhi ya Makuyuni Wildlife Park, iliyopo takribani kilomita 70 kutoka Jiji la Arusha, imeendelea kung'ara katika kurasa mbalimbali za habari za utalii duniani baada ya kupokea ugeni mzito wa Miss World China 2021 Bi Jiang Sigi, aliyetembelea hifadhini hapo Oktoba 11, 2025 akiwa ameambatana na washindi wa tuzo ya Miss Travel kutoka Hong Kong - China, Kenya na Tanzania.




Ziara hiyo maalum ya siku moja, iliyoratibiwa na kampuni ya Miss Travel World Beauty Pageant T/A Skyvfree International) chini ya kampuni mama Goshen Safaris, ililenga kuwapa wageni hao wenye ushawishi mkubwa katika nchi zao fursa ya kushuhudia vivutio vya utalii vilivyopo Makuyuni, na Kupitia majukwaa yao ya kimataifa, wageni hao wanatarajiwa kusaidia kuitangaza kwa kuionesha dunia jinsi Makuyuni Wildlife Park inavyozidi kuwa kivutio cha Kimataifa cha utalii wa wanyamapori, mandhari na utamaduni wa asili.



Akizungumza baada ya ziara hiyo, Mkurugenzi Mratibu wa Miss Travel World - Tanzania, Samweli Mulugu alisema kuwa hatua hiyo ni sehemu ya jitihada endelevu za kukuza utalii wa Tanzania kupitia wageni mashuhuri wenye ushawishi mkubwa katika nchi zao. Aliongeza kuwa kupitia ugeni huo, Hifadhi ya Makuyuni Wildlife Park itaendelea kujulikana zaidi katika soko la kimataifa na kuvutia wawekezaji wa sekta ya utalii.




Aidha, alitoa pongezi kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kwa juhudi zake katika kuendeleza utalii endelevu, kuhifadhi urithi wa asili, na kulinda tamaduni za jamii jirani.

Kwa upande wake, aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi upande wa Utalii–Kanda ya Kaskazini, Segoline Tarimo, aliishukuru kampuni ya Goshen Safaris kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutangaza vivutio vya utalii vya nchi yetu kupitia filamu za Tanzania The Royal Tour na Amazing Tanzania.

Pia aliwakaribisha wageni kutoka ndani na nje ya nchi kutembelea Hifadhi hiyo ili waweze kujionea vivutio mbalimbali vya utalii.

Wakati wa ziara hiyo, wageni walipata fursa ya kujionea wanyamapori mbalimbali m wakiwemo tembo, twiga, swalapala, choroa (oryx), pundamilia na wengine wengi, sambamba na burudani za ngoma za jadi za Kimasai.

Kutokana na kuvutiwa na mandhari na vivutio vya hifadhi hiyo, wageni hao walieleza azma yao ya kurejea tena Makuyuni Wildlife Park kwa ajili ya kufanya utalii wa kupanda vilima (hiking) na kuendelea kutangaza vivutio vya Tanzania kwa dunia.

# ZAIDI YA WAGENI 140 KUTOKA MATAIFA MBALIMBALI WATEMBELEA HIFADHI YA KILWA KISIWANI

*Na Beatus Maganja, Dar es Salaam*






Hifadhi ya Urithi wa Utamaduni wa Dunia ya Magofu ya Kale ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara wilayani Kilwa imeendelea kuwa kivutio kikubwa kwa watalii kutoka ndani na nje ya nchi, ambapo tarehe 31 Oktoba 2025 ilipokea jumla ya watalii 147 kutoka mataifa mbalimbali duniani waliowasili hifadhini humo kwa kutumia meli ya kifahari iitwayo SH Diana, kwa lengo la kutalii na kujionea vivutio vya kihistoria vilivyopo katika eneo hilo.

Watalii hao walitoka katika nchi 13 zikiwemo Ufaransa, Australia, Ubelgiji, Canada, Uingereza, Uswisi, Ujerumani, Cyprus, New Zealand, Marekani, Urusi, Uturuki na Ukraine. Ziara hiyo iliratibiwa na kampuni za Savannah Tours Ltd kwa kushirikiana na Black Willow Safaris.

Akizungumza wakati wa mapokezi ya watalii hao, Kamanda wa Hifadhi hiyo, Mhifadhi Mwandamizi Kelvin Stanslaus, alisema ujio wa wageni hao ni ishara njema kwa ukuaji wa utalii wa urithi nchini, hasa ikizingatiwa umuhimu wa Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kama maeneo yaliyosajiliwa na UNESCO kuwa Urithi wa Dunia tangu mwaka 1981.

"Tunayo furaha kubwa kuona wageni kutoka pande mbalimbali za dunia wakija kujionea historia adhimu ya Kilwa, ambayo ni alama muhimu ya biashara ya kimataifa ya karne za kati kati ya Afrika Mashariki na Dunia," alisema Afisa huyo.

Aidha, wageni hao walipata fursa ya kutembelea majengo ya kihistoria ikiwemo Msikiti Mkongwe, na Kasri la Sultani, ambapo walivutiwa na usanifu wa majengo ya mawe pamoja na simulizi za kihistoria zinazoambatana na maeneo hayo kutoka Kwa Maofisa wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA waliobobea na kutopea katika masuala ya malikale.

Kwa mujibu wa TAWA ambayo ndiyo wasimamizi wa hifadhi hiyo, ujio wa meli hiyo ni sehemu ya mwendelezo wa jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuimarisha utalii wa urithi, hususan katika maeneo ya bahari, malikale na visiwa vyenye thamani ya kihistoria.








# HIFADHI YA MPANGA-KIPENGERE YAENDELEA KUWA LULU YA VIZAZI VIJAVYO

*Na Beatus Maganja, Njombe.*

Wahenga walioshiba tunu za uhifadhi na utalii nchini waliwahi kusema "Kama unataka kujua uzuri wa Tanzania tembea ndani ya moyo wake, na moyo huo ni Hifadhi zake". Wengine walisema "Kuna safari ambazo hubadilisha mawazo, na kuna nyingine zinazogusa mwili, nafsi, moyo na roho".

Kuna mahali duniani ambapo miamba huzungumza Kwa sauti ya utulivu, mito ikiimba nyimbo za kale na upepo ukiandika mashairi yasiyofutika juu ya majani ya kijani, mahali ambapo asili huvaa vazi za kizalendo, mahali ambapo historia ikiishi, elimu ikitembea na Tanzania ikitabasamu. Hapa ndipo unapoikuta Hifadhi ya Mpanga-Kipengere, hifadhi iliyopo Mikoa ya Mbeya na Njombe ikiwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA.

Novemba 7, 2025 TAWA tulishuhudia ukurasa mwingine mzuri wa historia ya elimu na uhifadhi ulioandikwa ndani ya Hifadhi hii, wakati walimu na wanafunzi wa shule ya Sekondari Lupalilo kutoka Mkoa wa Njombe walipoitembelea Kwa ziara ya kujifunza na kutalii.

Ziara hii si safari ya kawaida, bali mwendelezo wa hamasa inayofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia TAWA inayosisitiza dhana ya "Tumerithishwa Tuwarithishe" lakini pia dhana ya "Tembea Tanzania, Jifunze Tanzania" dhana za utalii wa ndani zilizovuka mipaka ya starehe na kuwa chombo cha elimu, uchumi na uzalendo.
Kwa miaka kadhaa sasa, Shule ya Lupalilo imekuwa

mfano wa Kuigwa Kwa kuleta wanafunzi Mpanga-Kipengere, Si Kwa kutazama tu mandhari yake, bali kujifunza Kwa macho, miguu na akili. Mahali ambapo kila mwamba ni somo, kila korongo ni darasa na kila chemichemi ni nukuu ya uumbaji.



Ni Hifadhi pekee nchini ambapo mwanafunzi huweza kushuhudia miamba yote mitatu ya sayansi ya jiolojia. Mwamba moto, mwamba tabaka na mwamba geu.

Lakini Mpanga-Kipengere haizungumzi tu jiolojia, bali ni kitovu cha urithi wa historia ya Tanzania, mahali ambapo bado yanapumua majina makubwa ya Chifu Mkwawa Mkwavinyika na Chifu Merere, mashujaa waliotetea ardhi hii kabla haijawa hifadhi wakiamini kuwa nchi bila heshima ya ardhi yake ni nyumba isiyo na msingi.

Kupitia ziara kama hizi, vijana wanajengewa moyo wa uzalendo, kupenda mazingira na kuthamini rasilimali za taifa. Ni mahali ambapo vizazi vinalelewa si tu kuwa wasomi, bali walinzi wa urithi wa Tanzania.

Kwa maneno mafupi, Hifadhi ya Mpanga-Kipengere ni darasa liliandikwa Kwa mikono ya Muumba mwenyewe, ni darasa la uhai,mahali ambapo kila mgeni huondoka na zawadi inayoonekana Kwa macho ya nyama, zawadi ya kutua msongo wa mawazo na kuongeza upendo Kwa nchi yake, mahali ambapo mgeni huondoka akiwa amebeba zaidi ya kumbukumbu na ndoto mpya, ndoto ya kizazi kinachotambua kuwa utalii ni darasa, na uhifadhi ni urithi.



# TABORA ZOO YAENDELEA KUPOKEA MAKUNDI MBALIMBALI YA WATALII

*Na Beatus Maganja, Dar es Salaam*

Ikiwa zimesalia siku chache kuelekea kufunga mwaka wa 2025, Bustani ya Wanyamapori Hai Tabora, maarufu Tabora Zoo, Hifadhi inayotajwa kubeba historia iliyopea Kwa vipeo inaendelea kuwa kivutio cha makundi mbalimbali ya watalii wanaofika kwa ajili ya shughuli za utalii, mafunzo na kubarizi.

Mnamo Novemba 8, 2025, Umoja wa Akina Mama Mahiri (MMN) kutoka Wilaya ya Sikonge ulifanya ziara maalum katika bustani hiyo ili kujionea vivutio vya kipekee vya utalii vinavyopatikana ndani yake ikiwemo mandhari ya asili pamoja na wanyamapori hai kama tembo, nyumbu, hasa "nyumbu mwongozo wa watalii", ngiri maarufu "Kasongo", simba, chui na duma, sambamba na spishi mbalimbali za ndege nyuni wakiwemo tausi na kasuku mapenzi, wanaopamba anga la Mkoa wa Tabora kwa sauti na rangi zao za kuvutia.

Kwa kipindi cha hivi karibuni, Tabora Zoo imejipatia umaarufu mkubwa na kuwa kimbilio la watalii wengi kutoka ndani na nje ya mkoa huo. Hii ni kutokana na ongezeko la wanyamapori hai pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya utalii uliofanywa na Serikali kupitia TAWA, ikiwemo eneo la michezo ya watoto linaloongeza burudani na furaha kwa familia na wageni wanaotembelea bustani hiyo.

Aidha, TAWA inaendelea kuwakaribisha wananchi wote kutembelea hifadhi hiyo, ikiwemo taasisi za serikali, taasisi binafsi, vikundi vya vikoba, vyama na mashirika mbalimbali, kwa ajili ya vikao, mafunzo, sherehe za harusi na shughuli nyingine za kijamii zinazoambatana na utalii.











# DKT. ABBAS AHAMASISHA WAKAZI WA DAR ES SALAAM KUSHIRIKI TAMASHA LA FUNGA MWAKA KIJANJA TALII

*Na Beatus Maganja, Dar es Salaam*

TAMASHA la Funga Mwaka Kijanja Talii Msimu wa Pili linaloendelea katika viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam limeelezwa kuwa fursa muhimu kwa wakazi wa jiji hilo na Watanzania kwa ujumla kufanya utalii wa ndani kwa kushuhudia vivutio mbalimbali vya wanyama pori.

Tamasha hili lililoanza Disemba 2025 na kutazamiwa kufikia tamati Januari 05, 2026 ni sehemu ya kampeni kubwa ya kitaifa ya kuhamasisha utalii katika kipindi cha sikukuu na kufunga mwaka likiwa limeandaliwa na kuratibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii Kupitia Bodi ya Utalii Tanzania.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea tamasha hilo mapema leo Disemba 24, 2025, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas ametoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi katika tamasha hilo ili kuweza kupata elimu ya namna ya kuwekeza katika sekta ya utalii nchini, namna ya kushiriki katika biashara ya nyara na kupata kitoweo cha nyamapori kwa njia halali sambamba na kujionea wanyamapori hai wa aina mbalimbali wakiwemo tembo na ngiri maarufu "Kasongo yeye"

"Tunawaomba wananchi wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani waje viwanja vya SabaSaba Kilwa"Road" kujionea wanyamapori hai, mimi mwenyewe nimejionea Simba, duma, tembo, "Kasongo" (ngiri) pia yupo hapa" alisema Dkt. Abbas

Aidha Katibu Mkuu huyo amesema sekta ya utalii nchini iko imara, haijatikisika na inaendelea kuonesha ukuaji mkubwa licha ya changamoto mbalimbali zilizoikumba dunia na nchi yetu huku akibainisha kuwa kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu, idadi ya watalii imeongezeka kwa asilimia 9 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024 na kusisitiza kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kufanya vizuri katika eneo hilo.

"Watalii wameongezeka Tanzania kwa asilimia 9 kati ya mwezi Januari mpaka mwezi Novemba 2025. Kwahiyo kitaifa tunalo ongezeko la watalii laki moja na sabini na tatu (173,000) ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka jana" alisema Dkt. Abbas

"Hata kwenye taasisi yetu ya TAWA, wanafanya vizuri sana, utalii unafanya vizuri. Kwa takwimu za TAWA watalii wameongezeka kwa asilimia takribani 18 wa kutoka nje ya nchi na wale wa ndani wameongezeka kwa asilimia 40" aliongeza Dkt. Abbas

Dkt. Abbas ameongeza kuwa ongezeko hilo linatokana na jitihada za serikali katika kutangaza utalii, kuimarisha miundombinu na kuhakikisha usalama katika hifadhi zote nchini, huku watalii wa ndani na wa nje wakiendelea kuongezeka.
Kwa upande wake, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA Mlage Yussuf Kabange amesema lengo la kuanzisha tamasha hilo ni kuitikia maombi ya wananchi ya kutaka kupata wasaa mzuri zaidi wa kuona wanyamapori, maombi yaliyokuwa yakitolewa na wananchi katika kipindi cha maonesho ya biashara ya Kimataifa.

"Wakati tunafanya maonesho ya SabaSaba hapa, baadhi ya wananchi walileta maombi kwamba muda wa kuona wanyamapori hautoshi, sasa tukaona tuje na mikakati tofauti mkamati mmojawapo ni huu wa kuleta wanyama hawa wakati wa kipindi cha likizo ambapo wanafunzi watakuwa na nafasi ya kutosha na wazazi wao kuwasindikiza kuja kuona wanyamapori hawa" alisema Kabange

"Sasa ni kama tumehamisha mbuga kwa kuitoa porini na kuileta Dar es Salaam, kwakuwa tumeongeza wanyama ambao hawakuwepo katika maonesho mbalimbali yaliyopita ambao wananchi walihitaji wawepo kama vile tembo, ngiri na aina nyingine ya swala" aliongeza Kamishna Kabange





# MATUKIO KATIKA PICHA










## TAWA MICHEZONI

TAWA iliweza kushiriki kikamilifu katika mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika mnamo mwezi Novemba 2025, katika Mashindano hayo TAWA iliweze kushiriki katika Mpira wa Miguu, Riadha, Kuvuta Kamba Pamoja na Mpira wa Pete. Katika mashindano hayo TAWA iliweza kuibuka Mshindi wa Tatu (3) katika Mchezo wa Kamba na Mshindi wa Pili (2) katika Mbio za Mita 400.

# FUNGA MWAKA KIJANJA NA TAWA



Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA iliandaa Tamasha kubwa laKitalii la kufunga mwaka 2025 na kuukaribisha Mwaka Mpya 2026 lilijulikana kama "FUNGA MWAKA KIJANJA NA TAWA" lililofanyika katika Viwanja vya Maonesho ya Kimataifa ya Kibiashara (Sabasaba) kuanzia tarehe Disemba 20,2025 hadi Januari 5, 2026.

Tamasha hilo lilinogeshwa na uwepo wa wanyamapori hai wakiwemo Tembo, Simba, Chui, Twiga, Ngiri (Kasongo), Fisi na ndege wa aina mbalimbali akiwemo Mbuni. Pia wananchi walipata fursa ya kupata taarifa sahihi za maeneo ya uwekezaji na vivutio vya utalii vinavyosimamiwa na TAWA, kununua nyara za wanyamapori kama vile pembe, ngozi na mikia, sambamba na kupata kitoweo cha nyamapori.







tawa_tanzania

tztawa

Tanzania Wildlife Management Authority

TAWA TANZANIA

www.tawa.go.tz

Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA

Limetolewa Na;
Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA)
Eneo la Kingolwira, Barabara ya Dar es Salaam, Jengo la TAFORI,
S.L.P 2658, Morogoro.